

Lindi Islamic Foundation of Tanzania

MSINGI WA ASASI ZA KIISLAMU LINDI TANZANIA

**RATIBA YA SEMINA YA WALIMU WA
MADRASA NA IMAMU WA MISIKITI
TAREHE 05-APR-2015**

Ajenda



MUDA	MAELEZO	MUHUSIKA
2:00 -2:30 Asubuhi	USAJILI	KASSIMU NJONJORO
2:30 -2:45 Asubuhi	MAKARIBISHO	KASSIMU NJONJORO
2:45 -3:00 Asubuhi	KUFUNGUA KWA DUA	IMAM SAID (MASJID NUR)
3:00 -3:15 Asubuhi	UTAMBULISHO WA LIFT	MAHAMOODY NYIHRAN
3:15 -3:45 Asubuhi	DAAWAH	KASSIMU NJONJORO
3:45 -4:15 Asubuhi	AFYA	DR. HAMIS AJALI
4:15 -4:45 Asubuhi	CHAI	WOTE
4:45 -5:15 Asubuhi	ELIMU	ALLY SEIF
5:15 -5:45 Asubuhi	MAJADILIANO	WOTE
5:45 -6:00 Asubuhi	KUFUNGA KWA DUA	HOTUBA YA MGENI RASMI

USAJILI

UFUNGUZI NA UTAMBULISHO




UTANGULIZI

ALHAMDULILLAH-NLADHII-
HADANALIHADHA

WAMAAKUNNALIYAHATTADIYA-LAULA
ANN HADANALLHA THUMA waswalatu
wassalaam ghalaa sayyidina Muhammad
nurul hidayyatu waala alihii waswahabihi
wa mantabahu hum bil hisan illa
yaumidin.Amma baadu

NENO LA UKARIBISHO



Matayalisho na maandalizi ya hakika kwa ajili ya safari ya Akhera.

Qur:”Enyi mulioamini muogopeni m/mungu haki ya kumuogopa na wala musife isipokuwa mumekufa mukiwa waislamu kamili”

Qur: “ Enyi mlilioamini mcheni m/mungu na muzikague nafsi zenu zimetanguliza nini kwa ajili ya jambo la kesho Akhera”
Mtume (s.a.w) anasema “Zihesabuni nafsi zenu kabla bado hazijahebiwa”



KAUTHAR

Mtume s.a.w anawakaribisha waumini katika BIRIKA lake (Hodhi) waumini wa kweli wataiendea birika hiyo. Atakayekunywa katika birika hiyo hatopata kiu baada yake asilani. Kila mtume anabirika, kubwa zaidi ya hizo ni ya bwana Mtume Muhammad (s.a.w) Maji yake ni meupe zaidi kuliko maziwa, matamu zaidi kuliko asali na yananukia zaidi kuliko miski. Vyombo vyake ni dhahabu na fedha kama idadi ya nyota. Urefu wake ni wa mbali zaidi kuliko kutoka Aila huko Jordan mpaka Aden (Yemen) maji yake yanatoka katika mto KAUTHAR.

Allahuma jaalina min hum!



UTAMBUZI

Makusudio ya semina

WALIOHUDHURIA

Mkono kwa mkono hadi peponi.



Wabillahi Tawfiq

KUFUNGUA KWA DUA

UTAMBULISHO WA LIFT



“LIFT ni Asasi ya kidini, shirika la hiari ambalo halihusiani na siasa lililosajiliwa chini ya sheria ya mashirika ya jamii namba 337 R.E ya mwaka 2002 ambayo ilikuwa inajulikana kama sheria ya mashirika ya jamii namba 337 ya mwaka 1954.”



DHIMA YETU

Kuimarisha ubora wa Waislamu ki maisha katika mkoa wa Lindi kwa njia ya maboresho katika afya na elimu.

To enhance the Muslims quality of life in Lindi Region through improvements in health and education.



DIRA NA MAADILI YETU

LIFT inalenga kuwa shirika **sikivu**, **wazi**, na **ambalo** hutoa kwa wakati na kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, chakula na maji kwa waislamu WOTE, wanaoishi ndani ya mkoa wa Lindi-Tanzania. LIFT inaamini kuwa kila wafadhili wachangiaji na mchangiaji lazima aheshimiwe, na wote ni wenye thamani kwa kila mmoja. LIFT itazingatia viwango vya juu vya maadili ya quran na suna za Mtume Mohamad (S. W. A)


LIFT aims to be a **responsive**, **transparent**, and **agile** organization that provides timely and improved access to quality health care, food, education, and water to ALL people residing within Muslim communities in the Lindi Region of Tanzania. LIFT believes every donor, volunteer, and recipient must be respected; and, they are all valued customers to each other. LIFT strives to adhere to the highest ethical standards: the Quran and the Sunnah of Prophet Mohamed (PBUH).



MALENGO YETU

1. Kutoa msaada wa dharura wa chakula kwa wazee, walemavu, na wengine wanaoishi katika mazingira magumu ambao ni wakazi wa mkoa wa Lindi.
2. Kusaidia jamii katika kuanzisha huduma za afya stahili na salama.
3. Kuwasaidia watoto kupata elimu bora za diniya kiislamu na kidunia
4. Kusaidia jamii katika kupata maji ya bomba na endelevu
5. Kusaidia jamii katika kujenga miundombinu na kuboresha usafi.
6. Kukuza mazoea ya usafi salama
7. Kuchangia kwenye taasisi za kiislamu, misikiti kwa ajili ya elimu ya kiislamu, misingi ya Quran, suna na hadithi halisi.

MUUNDO WA UONGOZI



DAAWAH



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الحمد لله نحمده ونستعينه ونستغفره ونستهديه ونعوذ بالله من شرور أنفسنا ومن سيئات
أعمالنا من يهده الله فهو المهتد ومن يضله فلا هادي له وأشهد أن لا إله إلا الله الواحد الأحد
الفرد الصمد الذى لم يلد ولم يولد ولم يكن له كفواً أحد وأشهد أن محمدا عبده ورسوله أرسله
بألهدى ودين الحق ليظهره على الدين كله ولو كره المشركون اللهم صل وسلم عليه وعلى آله
وأصحابه أجمعين أما بعد




Baada ya kumshukuru Allah (s.w.) na kumtakia rehenia na amani mbora wa viumbe kipenzi chetu sayyidina Muhammad (s.a.w.).

Ningependa kuchukua fursa hii vilevile kwa kuwaombea dua Allah (S. W.) awapeni subira

Watukufu waislam nimepewajukumu la kuhudhurisha maada isemayo:-

QUR'AANI MUONGOZOKWA WANAADAMU



القرآن هدى للناس

Watukufu waislam:-

Qur' an ni neno la kiarabu kama maneno mengine ya lugha mbalimbali ambayo yanakua na maana ya kilugha na ya kiistwilaahi. Na neno hili nalo linamaana ya kilugha na kiistwilaahi. Kilugha neno **QUR' AN** lina maana ya kisomo au chenye kusomwa kama alivyo serna Allha (s.w)

فَإِذَا قَرَأْتَهُ فَاتَّبِعْ قُرْآنَهُ

Tutakapo kusomea fuata kisomo chake (75;18)




Amma Kiistilah:- Ni kitabu ambacho Allah (S.W) Amekiteremsha kwa Mtume Muhammad (S.A. W) ambacho katika majina yake ni pamoja na :- FUR- QAAN, KITAABUN, TANZIYLUNNA TIBYAANUN.

Kushughulika QURAAN katika kuisoma kuhifadhi na kuisomesha ni katika vitu ambavyo uislamu umevihimiza kupitia QUR' AN yenyewe na hadithi za bwana mtume (s.a.w) hata historia ya mzima ya uteremkaji na uhifadhi wa QUR' AN (73:4)

Kabla hatujaingia kwenye fadhila na faida za kushughulikia QUR' AN ebu tuangalie kwanza hatua ambazo QUR' AN imepitia katika kukusanywa kwake mpaka kufikia hapa tulipo tunaisoma ikiwa misahafu na mahala penginepo.

UKUSANYW AJI W A QUR' AAN



Ukusanywaji wa QUR' AAN umepitia katika hatua nne maarufu ambazo ni:-

1. Kuhifadhi QUR'AAN katika vifua *حفظ القرآن في الصدور*
2. Upangaji wa surah za QUR' AAN '
3. Upangaji wa aya katika surah za QUR' AAN
4. Uwandikaji wa QUR'AAN katika suhufna misahafu



Ukusanywaji wa kwanza ulifanyika katika wakati wa mtume (s.a.w) kipindi ambacho QUR' AAN ilikua inateremshwa kwa mtume (s.a.w) alihifadhi kifuani QUR' AAN yote pamoja na baadhi ya maswahaba hali hiind

Pamoja na ukusanywaji huu mtume (s.a.w) aliwaweka watu maalumu wa kuandika wahyi ambao wanafahamika kama

كتاب الوحي

Nao ni akina Ubayyu Ibin Kaabi, Muaadhi Ibin Jabal, Zaid Ibin Thaabit na Abuu Zaid Ama ukusanywaji wa pili ni upangaji wa surah za QUR' AAN katika Msahafu kama vile kuanza na Suuratul-faatiha kisha suurah saba ndefu

السبع الطوال

Kasha zikafuatia suurah ndefu kidogo hii ni kazi iliyo fanywa na maswahaba wa mtume.




Kuna ukusanywaji wa tatu ambao ni upangaji wa aya za QUR'AAN Qur'an ilikua inateremshwa kwa vipande vipande laikini si kwamba mpaka suurah moja iishe ndipo ianze nyigine laa isipokua wakati surah moja inateremka kabla haijaisha inaweza ikateremka suurah nyingine au kipande cha sura nyingine. Kwahiyo mtume (s.a.w) alikua anabainisha kua aya hizi ni za sehemu flani katika suurah flani



Kuna ukusanywaji wa nne ambao ni uandikaji wa Qur'aan kwa suhufna msahafu nao umegawanyika katika sehemu mbili:-

1. Hatua ya kwanza ilikua kukusanya Qur'aan ambayo imetawanyika na kuiweka kwenye suhuf (vitabu) kazi ambayo ilifanywa na Abuubakari sswiddiyq (r.a)
2. Sehemu ya pili ya ukusanywaji huu ni kukusanywa zile suhufna kuziweka pamoja na kupatikana Muswahafu (msahafu) ikiwa na maana suhufu zilizo kusanywa pamoja. Kazi iliyofanyw na sayyidina Uthmaani (r.a)



Kuna sababu zilizopelekea Abuubakari aikusanye Quran. Vilevile kuna sababu zilizo mpelekea Athmani aikusanye kwa mara yapili katika msahafu.

Abuubakari aliikusanya Qur'an na kuiweka katika suhufkwa khofu ya kupotea kutokana na kufa kwa maswahaba wengi katika vita vya yamaam inakadiriwa maswahaba karibu 660 walikufa katika vita hivyo.

Na Othmani aliikusanya Qur'an katika msahafu mmoja ili watu wasitofautiane katika usomaji kitu ambacho kilisha tokea

Haya yote ambayo nimeyaeleza ni kuwaonyesha kwa kiasi gani Mtume na Maswahaba walikua na tahadhari juu ya hii QUR' AAN isipotee.



Kazi ambayo sasa hi vi ipo mikononi !pwenu Walimu, Maimamu, Maamiri, Makhalifa na Waislamu kwa ujumla.

Katika kulisimamia hili kuna fadhila kubwa za kidunia na Akhera. Na miongoni mwa sifa za umma huu ni jambo hili la uhifadhi wa QUR' AAN - kama alivyosema mwanachuoni WAHBU IBNI MANBAHI akielezea umma huu kwamba ni:-Umma ambao vitabu vyao vimo nyoyoni mwao.



Abu Saidil- Khudriyyi amesema amesikia Mtume S. A. W akisema:-
Ataambiwa mwenye QUR' AANI atakapoingia peponi soma na
panda atasoma na atapanda daraja kwa kila aya ambayo atasoma
mpaka atapofika aya ya mwisho kuisoma .


Hapana budi tujipinde kwa kiasi kikubwa ili kuweza kuzifikia daraja
hizo pamoja na kumuomba Allah S.W atuwezeshe

اللهم ارزقنا تلاوة كتابك حق تلاوة واجعلنا ممن نال به الفلاح والسعادة اللهم ارزقنا إقامة
لفظه ومعناه وحفظ حدوده ورعاية حرمة الله اجعلنا من الراسخين في العلم المؤمنين بمحكمه
ومتشابهه تصديقاً بأخباره وتنفيذاً لأحكامه واغفر لنا ولوالدينا ولجميع المسلمين برحمتك يا أرحم
الراحمين وصلى الله على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين آمين
والسلام عليكم ورحمة الله وبركاته.

Qur`an Ni Muongozo


Imeandaliwa na LIFT Kamati ya Afya

Assalam alaykum



Bismillah Rahman Rahim

Yaliyomo



- Utangulizi
- Mifano mbalimbali
- Mwanadamu azingatie nini



Utangulizi

- Qur`an ni mwongozo kama anavyosema Mwenyezi Mungu `Hicho ndicho kitabu, kisicho na shaka ndani yake – ni muongozo kwa wamchao Mwenyezi Mungu (2:2)
- Kama ukiwafikieni mwongozo utokao kwangu basi watakaofuata muongozo wangu haitakuwa hofu kwao wala hawatahuzunika (2:38)



- Pia Mwenyezi Mungu anasema `hatukupuuza ndani ya kitabu hichi (kutaja) chochote ` (6:38)



Mifano mbalimbali



Unyonyeshaji

- Imehimiza na kuelekeza masuala ya unyonyeshaji kwa kusema
- `Na wanawake waliozaa wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kwa anaetaka kukamilisha kunyonyesha` (2:233)
- Wataalamu wa dunia leo wamekiri kuwa maziwa ya mama ni muhimu sana kwa ukuaji wa mtoto kimwili na kiakili



Maji na Mazoezi kama tiba

- Mwenyezi Mungu anasema `Mkumbuke mtumishi wetu Ayubu alipomwita Mola wake, akinena kwa yakini shetani amenifikishia udhia na taabu (38:41)
- Mwenyezi Mungu akamjibu, `Kaza mwendo, hapa mahali baridi pa kuogea na kinywaji` (38:42)
- Kwahiyo alielekezwa afanye mazoezi na atumie maji kwa ajili ya kutibu homa aliyonayo.



- Wajapani nao hutumia maji (Water Therapy) kwa kutibu maradhi mbali mbali kama vile BP, Kisukari N.k.



- Bi Mariam alipojifungua chini ya mtende
- Mara ikamfikia sauti kutoka chini yake, usihuzunike. Hakika Mola wako ameweka kijito chini yako (19:24)
- Hii inaonyesha umuhimu wa maji kwa ajili ya usafi

Chakula



- Enyi watu! Kuleni katika vile vilivyomo ardhini, vilivyo halali na vyenye kufaa kiaafya ... (2:168 na 5:88)



Pombe na Kamari

- `Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: katika hivyo mna dhambi kubwa na manufaa kwa watu pia, lakini dhambi yake ni kubwa zaidi kuliko manufaa yake` (2:219)
- Madhara ya pombe, mtume amesema `Mwislamu anapokunywa pombe imani inatoweka` (Bukhari)
- Pombe ni mbegu ya maovu mbali mbali
- Pombe inaleta magonjwa mbalimbali, kama ugonjwa wa ini



Madhara ya pombe

- Majeraha
- Kukosa nguvu za kufanya kazi
- Ulevi unapunguza maisha
- Uhai unaotazamiwa na watu wasiokunywa ni mara mbili ya ule wa watu wanaolewa
- Uhalifu wa sheria 25 – 85% ni walevi
- Mtoto wa mlevi huathirika kimwili na kiakili
(Jewish Encyclopaedia I, 333 – 334, pia tazama Encyclopaedia Britannica 14th Edition, 540)



Madhara ya Kamari

- Kamari ni njia isiyohalali ya kuchuma mali ambayo inaleta chuki, ugomvi, uuaji na umaskini.



Nini Mwanadamu afanye

- Aisome qur`an na kuifuata atafanikiwa inshallah



Wabillahi Tawfiq



Mapumziko ya Chai-15 dakika



NAFASI YA MWALIMU KATIKA UISLAMU

UISLAMU UNASEMAJE KUHUSU ELIMU?



MAANA YA ELIMU

- ELIMU NI UJUZI AU UTAMBUZI WA MAMBO
- ELIMU NI UFAHAMU WA MAMBO
- ELIMU NI MWANGAZA WA KUMUWEZESHA BINADAMU KUFANYA MAMBO YAKE KWA UFANISI
- ELIMU NI NYENZO YA KUMUWEZESHA BINADAMU KUYAMUDU MAZINGIRA YAKE VIZURI

NAFASI YA ELIMU KATIKA UISLAMU



- NI AMRI YA KWANZA KWA MWANADAMU SURATUL BAQARA (KISA CHA NABII ADAM NA MALAIKA)
- NI AMRI YA KWANZA KWA MTUME MUHAMMAD SWALLA LLAHU ALAYHI WASALLAM (SURATUL ALAQ)
- NI NURU KUTOKA KWA MWENYEZIMUNGU (SURATUL ALAQ)

NAFASI YA ELIMU KATIKA UISLAMU



- NI NYENZO YA KUMUWEZESHA MTU KUWA MCHAMUNGU (INNA MAA YAKHSHALLAHA MIN IBADIHIL ULAMAA)
- KI KIGEZO CHA UBORA WA MTU (HAL YASTAWIL LADHIINA WAL LADHIINA LA YAALAMUUNA?)
- NI SABABU YA MTU KUFANIKIWA DUNIANI NA AKHERA



NAFAFI YA MWALIMU MUISLAMU KATIKA JAMII

KWANINI MWALIMU MUISLAMU



MWALIMU MUISLAMU

- ANALJUA LENGU SAHIHI LA MAISHA YA MWANADAMU HAPA DUNIANI
- ANA MUONGOZO ULIO SAHIHI WA MAISHA
- ANAJUA LENGU LA ELIMU KWA WANADAMU
- ANAJUA DHIMA YA MWALIMU KATIKA JAMII
- ANAKUA MALIPO YA MWALIMU KATIKA JAMII

NAFASI YA MWALIMU KATIKA JAMII



- MWALIMU NI KIOO CHA JAMII
- MWALIMU NI KIONGOZI WA KIJAMII
- MWALIMU NI MLEZI WA JAMII
- MWALIMU NI KIUNGO KATI YA WAZAZI NA WANAFUNZI
- MWALIMU NI MREKEBISHAJI WA JAMII
- MWALIMU NI DA'IYA

MAJADILIANO

KUFUNGA KWA DUA